

CHUO CHA UFUNDI STADI TURNBULL MKOANI IRINGA

SIKU YA TURNBULL, 02/10/2025

MIAKA 8 YA MAFUNZO.

GEREZA LA PAWAGA

Chuo cha ufundi stadi Turnbull ni chuo kinachotoa mafunzo ya aina mbalimbali hapa mkoani Iringa na vilevile ni chuo ambacho kimesajiliwa na Serikali kwa usajili wa REG/NACTVET/0762-P. Pamoja na kutoa mafunzo ya fani mbalimbali chuo cha Turnbull mwaka 2023 kilianzisha mpango mkakati maalum wa kila mwaka siku ya Turnbull Tech College kuwa na matendo ya huruma ya kugusa makundi maalum ndani ya jamii yetu kama vile:-

- 1) Walemavu
- 2) Wagonjwa Hospitalini
- 3) Watoto Yatima na wenye mazingira magumu
- 4) Wajane na Wazee
- 5) Kutembelea Wafungwa Magerezani

Kwa muktadha huo basi, kwa kuendeleza mpango mkakati wetu wa kugusa makundi hayo chuo cha Turnbull mwaka huu 2025 kimejiwekea mkakati wa kutembelea **GEREZA LA PAWAGA** tarehe 02/10/2025 kwa neema ya Mungu.

Matendo yetu ya huruma kwa wafungwa wa GEREZA LA PAWAGA licha ya kufika katika gereza hili lakini kwa kushirikiana na wadau mbalimbali tunategemea kufanya matendo ya huruma kwa kutoa vitu vifuatavyo kadri Mungu atakavyotuwezesha kuvipata kutoka kwa Wadau wetu:

VITU TUNAVYOTEGEMEA KUTOA KWA WAFUNGWA WA GEREZA LA PAWAGA NI KAMA IFUATAVYO:-

S/No:	ITEMS	S/No:	ITEMS
1.	<i>SUKARI</i>	9.	<i>SABUNI ZA MCHE</i>
2.	<i>CHUMVI</i>	10.	<i>SABUNI ZA UNGA & ZA MAJI (Chooni & za kawaida)</i>
3.	<i>MICHELE</i>	11.	<i>DAWA ZA MENO NA MISWAKI</i>
4.	<i>UNGA WA UGALI</i>	12.	<i>VIFAA VYA USAFI (Mifagio, Ndo, Leki nk.)</i>
5.	<i>UNGA WA NGANO</i>	13.	<i>NETI (Vyandalua) na dawa ya kuulia wadudu</i>
6.	<i>TAULO ZA KIKE (PEDI)</i>	14.	<i>MAJI</i>
7.	<i>MAFUTA YA KULA</i>	15.	<i>VITABU VYA IMANI NA VITABU VYA KUELIMISHA</i>
8.	<i>MAFUTA YA KUPAKAA</i>	16.	<i>MAHARAGWE</i>

LENGO LA TUKIO HII NI KAMA IFUATAVYO:

- {1} Kuwatambua wafungwa kama sehemu ya jamii inayohitaji **faraja, upendo na msaada**
- {2} Kutoa msaada wa Kiroho kwa wafungwa ili kuwapa tumaini jipya
- {3} Kukuza moyo wa huruma na kujitoa kwa wanafunzi wetu, wadau wetu na jamii kwa ujumla

{4} Kujenga mahusiano mazuri kati ya Chuo na Jamii kwa kushirikiana katika kusaidia wenye uhitaji.

Tunatambua kuwa hatuwezi kufanikisha jambo hili pasipo msaada wa wadau na watu wenye moyo wa huruma kama wewe. Kwa heshima na taadhima, tunakuomba kushiriki nasi kwa namna yoyote ile utakavyoona inafaa, iwe ni kupitia msaada wa vitu tajwa hapo juu, fedha, au hata ushauri na uwepo wako wakati wa ziara yetu.

TAREHE YA ZIARA: 02/10/2025 –Gharama za usafiri zitatoka ofisini.

MAHALI: Gereza la Pawaga, Mkoani Iringa.

Tunaamini kuwa kwa pamoja tunaweza kuleta tabasamu kwa wale walioko gerezani, tukiwakumbusha kuwa bado wanapendwa na kuthaminiwa na jamii.

"Kusaidia ni kuonyesha upendo – na upendo hubadilisha maisha."

Tunatanguliza shukrani zetu za dhati kwa moyo wako wa upendo na msaada.

Barua pepe (E-Mail Address): info@turnbullcollege.ac.tz

Tovuti (Website) www.turnbullcollege.ac.tz

MAWASILIANO: 0623561873 AU 0622298845 AU 0734305992

KESHO YETU HATUIJUI!!

HIVYO

TUNAWAKARIBISHA SANA MATENDO HAYA YA HURUMA KWA WAFUNGWA